

Taarifa kwa Vyombo vya Habari.

Julai 14, 2017 Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Halima Dendego alihitimisha ziara yake ya siku Nne ya kukagua na kutembelea miradi ya maendeleo wilayani Nanyumbu. Akiwa katika Wilaya hiyo, Mhe. Dendego alijionea na kuridhishwa na hatua kubwa inayochukuliwa na Halmashauri hiyo katika kutatua changamoto mbalimbali katika jamii ikiwemo ongezeko la makusanyo ya fedha za ndani kutoka shingi 1,148,126,911 mwaka 2015/2016 sawa na 89% ya makisio hadi shilingi 1,783,650,621.80 mwaka 2016/2017 sawa na asilimia 100.43 ya makisio.

Katika kuongeza nguvu jitihada hizo Mhe. Dendego aliagiza majengo yaliyokuwa yakinumiwa na wakandarasi wa ujenzi wa barabara ya Mangaka-Mtambaswala yaliyoko kijijini Mtambaswala yabadilishwe na kutumika kama Kituo cha Afya, wakati yale yaliyoko Mjini Mangaka yatumike kama Shule ya Sekondari kidato cha Tano na Sita mchepuo wa Sayansi. Pia alikabidhi mbao 1100 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule na afya katika shule za Msingi Michiga B, Kazamoyo, Lidede na Masuguru. Pia zahanati ya Kazamoyo na Kituo cha Afya Mnanje.

Licha ya kushiriki moja kwa moja katika shughuli za maendeleo wilayani hapo Mhe, Dendego alitoa msaada na kuahidi kumalizia hatua mbalimbali walizozianza wananchi katika miradi mbalimbali ya maendeleo. Pia alikabidhi jumla ya mifuko ya saruji 250 kwa shule za Msingi Lidede, Sengenya na Zahanati ya Mikangaula na ahadi ya mabati 860 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa shule ya Msingi Lidede na kituo cha afya Mnanje.

Aidha, Mheshimiwa Dendego aliwataka wananchi wa wilaya ya Nanyumbu kutorudi nyuma katika jitihada walizozianza katika kukabiliana na changamoto wanazokutana nazo.

Imetolewa na;

Evaristy Masuha

Afisa Habari Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mtwara